# Jinsi ya Kuthibitisha na Kuchanganua Viambajengo na Muundo wa Virai

Deo S. Ngonyani


**Ikisiri**

*Makala hii inafafanua vigezo vya kubainisha viambajengo katika Kiswahili. Vigezo hivyo ni (a) ubadili, (b) usogezaji, (c) majibu mafupi na udodoshaji, na (d) uambatishaji. Vyote hutumika sana kama njia zilizojaribiwa za kutambua mipaka ya virai na viambajengo katika lugha mbalimbali duniani (Aarts, 2001; Carnie, 2012; Sportiche, Koopman, & Stabler, 2014; Haegeman, 2006). Umuhimu na matumizi ya vigezo hivyo unatolewa mfano kwa kuchunguza muundo wa sentensi, virai vitenzi vyenye yambwa mbili, na tungo tata. Matumizi ya mujarabu huu wa viambajengo ni nyenzo muhimu katika kutafiti lugha kwa mikabala yote. Ni mfano bora wa utafiti wa kisayansi ambao ni jarabati.*



## 1. Utangulizi

Yeyote ambaye amechunguza muundo wa sentensi katika Kiswahili, kadhalika muundo katika lugha nyingine, atakuwa amebaini mapema sana kwamba maana ya sentensi haitokani na kujumlisha maana ya maneno yaundayo sentensi. Sentensi si mfuatano tu wa maneno. Maana ya sentensi si jumla ya maana ya maneno yaundayo sentensi hiyo. Maneno huunda vikundi viitwavyo virai, virai navyo huunda vishazi na sentensi. Vikundi hivyo huitwa viambajengo. Tunapochanganua sentensi tunavitambua viambajengo hivyo na kudhihirisha kwa kutumia parandesi au vielelezo matawi. Lakini muundo wa viambajengo si kitu dhahiri.

Hebu tuangalie mfano mmoja rahisi wa uchanganuzi wa sentensi. Mfano huu unatoka kwa Besha (1994:95):

2 (a) Mtoto mmoja ameleta machungwa matamu.
(b) [$_{S}$ [$_{KN}$ mtoto mmoja] [$_{KT}$ ameleta [$_{KN}$ machungwa matamu]]][1]

1 Besha (1994) hakutumia parandesi katika uchanganuzi wake. Uwasilishaji huu wa parandesi ni tafsiri yetu ya kielelezo matawi hicho.




Mchanganuo huu unaonesha kwamba tungo hii imeundwa na vikundi au viambajengo viwili. Kikundi cha kwanza [*mtoto mmoja*] ni kirai nomino (KN). Kikundi cha pili [*ameleta machungwa matamu*] ni kirai kitenzi (KT). KT hiki kimeundwa na neno kuu la kirai [*ameleta*], neno ambalo ni kitenzi (T) pamoja na yambwa [*machungwa matamu*] ambacho ni KN. Mchanganuo huu hukubalika kwa wana sarufi ya Kiswahili[2].

Hata hivyo, tutathibitishaje kwamba mchanganuo huu ni sahihi na wala si kama huu ufuatao?


---

[2] Kielelezo cha vifupisho:

| | | | |
|---|---|---|---|
| E | Kielekezi | KE | Kirai Elekezi |
| H | Kihusishi | KH | Kirai Husishi |
| N | Nomino | KN | Kirai Nomino |
| T | Kitenzi | KT | Kirai Kitenzi |
| V | Kivumishi | KV | Kirai Vumisho |
| S | Sentensi | | |

Katika makala hii tunafuata desturi na mapokeo ya mpangilio na utoaji mifano kama ifanyikavyo katika majarida na vitabu vya isimu. Tunaonesha sentensi au virai visivyokubalikwa kwa kuweka nyota mwanzoni.

1 (a)




(b) [mtoto mdogo] [ameleta] [machungwa matamu]

Katika mchanganuo huu, sentensi imeundwa na matawi matatu, KN, T na KN. Kwa kweli mchanganuo huu unaendana vema kabisa na yale yanayozungumzwa kitipolojia. Yaani lugha ya Kiswahili ina muundo wa Kiima-Kitenzi-Yambwa. Kiima na yambwa katika sentensi hii ni virai nomino. Lugha nyingine zina muundo wa Kiima-Yambwa-Kitenzi, na nyingine Yambwa-Kitenzi-Kiima, na kadhalika. Je, tutathibitishaje uchanganuzi ulio katika **Error! Reference source not found.**) ni sahihi na 1) si sahihi?

Katika makala hii tutaonesha njia jarabati za kuthibitisha viambajengo na virai. Njia hizo hutumiwa na wanaisimu wa milengo na mikabala mbalimbali. Walimu na wanafunzi wa sarufi ya Kiswahili wataweza kuwa na nyenzo bora ya kufanyia utafiti na kuchunguza miundo ya Kiswahili kwa kutumia vigezo jarabati. Katika makala hii, tunakusudia kufanya mambo matatu muhimu katika kuendeleza stadi za uchambuzi wa sentensi kwa wanafunzi na wakufunzi wa Kiswahili na Isimu kwa jumla. Kwanza tunaelezea vigezo mbalimbali vya kubainisha viambajengo. Vigezo hivyo ni (a) ubadili, (b) usogezaji, (c) majibu mafupi na udodoshaji, na (d) uambatishaji. Mbinu hizi hutumika na wanaisimu wa mikabala mbalimbali kwa sababu zinakubalika kwa kiwango kikubwa sana kuwa ni njia jarabati za kubainisha viambajengo (Sportiche, Koopman, & Stabler, 2014; Carnie, 2013; Haegeman, 2006; Aarts, 2001). Pili, tutatumia mifano kutoka Kiswahili. Ijapokuwa mbinu hizi zinajulikana sana, matumizi yake katika kuchambua na kuchanganua miundo ya Kiswahili hayajawa makubwa. Makala hii inajaribu kuziba pengo hilo na kuhimiza matumizi ya hoja mujarabu. Tatu, tutaonesha kwa mifano halisi jinsi ambavyo hoja mujarabu zinavyoweza kutumika zaidi katika uchunguzi wa namna mbalimbali unaohusu

viambajengo vya Kiswahili na hata kutathmini nadharia mbalimbali mintarafu miundo mbalimbali.

Katika sehemu sita zijazo, tutaelezea vigezo hivyo na kutoa mifano. Baada ya sehemu hii ya utangulizi, tutaonesha jinsi vibadala vinavyoweza kutumika katika §2. Katika §3, tutaelezea uhamishaji au usogezaji. Majibu mafupi na udondoshaji ni mbinu zinazoelezewa katika §4. Njia ya mwisho tunayoijadili ni uambatishaji katika §5. Umuhimu wa mbinu hizi unaonyeshwa katika §6 ambapo tunatoa mifano kuthibitisha miundo ya sentensi, sentensi za kauli ya kutendea yenye yambwa mbili, na katika kuonyesha utata wa kimuundo. Hitimisho ni sehemu ya mwisho, yaani §7.

## 2. Matumizi ya Vibadala

Njia ya kwanza tunayoilezea hapa ni ubadili. Viambajengo vingi huweza kubadilishwa kwa kutumia maneno mbadala. Makundi ambayo hayaundi virai au viambajengo hayawezi kubadilishwa na maneno kama viwakilishi (Haegeman 2006; Radford 1988). Katika sehemu hii tutaanza kwa kutoa mifano ya kubadilisha virai nomino na kutumia viwakilishi, vikundi tenzi, vikundi husishi, na ubadili wa vishazi.

### 2.1 Vibadala vya Virai Nomino

Virai nomino hubadilishwa na viwakilishi hasa kama vikundi hivyo ni kiima. Kwa mfano, tunaweza kuona kikundi nomino cha kiima katika sentensi ifuatayo.

3 (a) *Mwanafunzi wa isimu* ameandika makala nzuri.
(b) *Yeye* ameandika makala nzuri sana.

4 (a) *Jambo lililotuudhi wanachama* liliwaudhi viongozi pia.
(b) *Hilo* liliwaudhi viongozi pia.

Katika sentensi **Error! Reference source not found.**a), kikundi nomino *Mwanafunzi wa isimu* kinabadilishwa na *yeye* katika **Error! Reference source not found.**b). Kadhalika katika **Error! Reference source not found.**a), kikundi nomino cha kiima *jambo lililotuudhi wanachama* kinabadilishwa na kiwakilishi onyeshi *hilo* ***Error! Reference source not found.***b). Ubadilishaji huu unawezekana tu tunapokuwa na kiambajengo. Tunapojaribu kutumia mbinu hii kupata viambajengo zaidi, tunagundua kwamba hatuwezi kupata viwakilishi iwapo kikundi cha maneno hakifanyi kiambajengo. Kwa mfano, [*Mwanafunzi wa isimu ameandika*] hakiwezi kubadilishwa na kiwakilishi.

2 (a) **Yeye* makala nzuri[3].
(b) **Hilo* viongozi pia.

Mifano hii inadhihirisha kwamba, [*mwanafunzi wa isimu ameandika*] si kiambajengo katika sentensi **Error! Reference source not found.**a) kwani kikundi hiki hakiwezi kuwasilishwa na *yeye*. Hali kadhalika, katika **Error! Reference source not found.**b) *hilo* ni kionyeshi kisichoweza kuwasilisha [*jambo lililotuudhi wanachama liliwaudhi*] kwa kuwa si kiambajengo.

Vikundi nomino huweza kubadilishwa na viwakilishi kulingana na nafasi na uamilifu wake katika kishazi. Hapa tutaangalia vikundi nomino katika nafasi tatu tofauti. Nafasi hizo ni: (a) kiima, (b) yambwa na (c) kijalizo cha kihusishi. Tutaangalia mifano ya kila moja.

### *2.1.1 Ubadili wa Kiima*

Katika Kiswahili, tunatumia kirai cha kiima pamoja na kiambishi cha upatanisho wa kisarufi kwenye kitenzi, kama tunavyoona katika mifano ifuatayo:

3 (a) Wageni waliondoka mapema.
(b) Mkulima alivuna mpunga.

Katika sentensi 3a), kitenzi *waliondoka* kina kiambishi awali *wa-* chenye kudhihirisha upatanisho wa kisarufi na kiima *wageni*. Hali kadhalika, katika 3b), kiima *mkulima* kinasababisha kuwapo kwa kiambishi awali *a-* katika *alivuna*. Wanaisimu kadhaa wameelezea kuridhishwa kwao kwamba, kiambishi awali hiki ni cha upatanisho wa kisarufi (hasa Bresnan na Mchombo 1987; Keach 1995). Kwa hivyo basi, tunapotaka kuwa na kiwakilishi kwa ajili ya kiima, tunaweza kutumia maneno kama *mimi, wewe, yeye, sisi, ninyi*, na *wao*. Tunatumia viwakilishi hivyo katika mifano hii:

4 (a) [*Watoto wa mgeni wetu*] waliondoka mapema.
(b) *Wao* waliondoka mapema.

5 (a) [*Mchezaji aliyewatukana waamuzi wa mchezo*] amefungiwa kucheza.
(b) *Yeye* amefungiwa kucheza.

---

[3] Wanasarufi wengine hawapendi kuangalia tungo ambazo si sahihi. Lakini, je, tutajuaje kwamba miundo fulani haikubaliki bila kuziangalia zisizo sahihi kwa namna ya majaribio? Isitoshe, hatuwezi kufahamu kikomo cha tungo sahihi. Tutaweza kujua mipaka ya miundo sahihi zile zilizopo na zile ambazo zingeweza kuwapo, zilizo sahihi na zisizo sahihi? Tunachofanya hapa kwa hakika ni kama majaribio ya kisaikolojia.

Katika 4), *wao* inasimama badala ya *[Watoto wa mgeni wetu]*. Sentensi 8 5b) ina *yeye*, ambacho ni kiwakilishi cha *[Mchezaji aliyewatukana waamuzi wa mchezo]*.

### *2.1.2 Ubadili wa Yambwa*

Yambwa huweza kuwakilishwa na kiambishi awali cha yambwa. Kwa kweli hatuoni sana matumizi ya viwakilishi huru vya kiima kama *yeye*, *wewe*, *wao*, nk. Vinapotumika hasa huwa ni katika kutia mkazo na sio kwa dhana ya uwakilishi hasa. Viambishi tulivyovitaja ndivyo vitumikavyo hasa kwa uwakilishi (Bresnan na Mchombo, 1987: Keach 1995). Tunaviona viambishi hivyo katika sentensi zifuatazo:


6 (a) Juma alinunua [*kile kisu cha kukatia miwa*].
(b) Juma alikinunua.

7 (a) Mama atajenga [*nyumba itakayowahifadhi yatima*].
(b) Mama ataijenga.

Kiambishi –*ki*- katika 6b) kinawakilisha *[kile kisu cha kukatia miwa]*. Hali kadhalika, kiambishi –*i*- kinawakilisha *[nyumba itakayowahifadhi yatima]* katika 7b). Endapo sentensi hizo zitarefushwa kwa kuongeza kielezi, tutaona mipaka ya kiambajengo.

8 (a) Mama atajenga nyumba itakayowahifadhi yatima mwaka kesho.

(b)



Virai hivi haviundi kiambajengo

Kielelezo matawi kinaonesha kwamba *[nyumba itakayohifadhi yatima]* na *[mwaka kesho]* haviundi kiambajengo bila ya kitenzi atajenga. Jambo hili linathibitishwa katika jaribio la kutumia kiwakilishi.

9 (a) Mama ataijenga ---- mwaka kesho.
(b) *Mama ata**i**jenga ---- ----.

Kwa kutumia kiambishi cha Ngeli ya 9 (ya *nyumba*), tunaweza kusema kama ilivyo katika 9a). Iwapo tutasema pasipo kirai elezi kama ilivyo katika 9b), maana ya kirai elezi haitaweza kushirikishwa katika kiwakilishi hicho. Sentensi hiyo ni sahihi kwa maana tofauti na hiyo tunayokusudia hapa.

### *2.1.3 Ubadili wa Yambwa za Vihusishi*

Baadhi ya yambwa za vihusishi huweza kujitokeza kama viangami. Kwa mfano, *na wao* huwa *nao, na hicho* huwa *nacho*, na kadhalika. Kiangami hiki pengine huoneka kama kiambishi cha upatanisho wa kisarufi. Matumizi yake tunayaona katika mifano ifuatayo.

10 (a) Wageni walizungumza [*na watu waliodai kuwa ni wenyeji wao*].
(b) Wageni walizungumza [*nao*].

11 (a) Askari wetu walipambana [*na kikosi cha mamluki kutoka msituni*].
(b) Askari wetu walipambana [*nacho*].

Katika sentensi 10a), *[watu waliodaiwa kuwa ni wenyeji]* ni kijalizo cha kihusishi *na*. Kijalizo hicho kinawakilishwa na *–o* katika *nao* 10b). Mfano mwingine ni huo 11a), ambapo *[kikosi cha mamluki kutoka msituni]* kinawakilishwa katika *nacho* 11b).

### 2.2 Ubadili wa Kirai Kitenzi

Kirai Kitenzi nacho huweza kuwasilishwa na maneno mengine. Hapa tunao mfano mzuri wa matumizi ya kiwakilishi oneshi *hivyo*. Twajua kwamba katika Kiswahili, viwakilishi onyeshi *hivi*, *hivyo* na *vile* hutumika kama vielezi pia. Katika mifano ifuatayo tunaonesha jinsi viwakilishi oneshi hivi vinavyotumika badala ya virai tenzi.

12 (a) Mgeni aliyeondoka *[alichukua vitabu vilivyobaki mezani]*.
(b) Nani alifanya *[hivyo]*?
(c) Mgeni aliyeondoka alifanya *[hivyo]*.
(d) *Mgeni aliyeondoka alifanya *[hivyo]* vilivyobaki mezani.

Katika sentensi ya 12b) na 12c) twaona kwamba kirai tenzi *[alichukua vitabu vilivyobaki mezani]* kinawasilishwa na *alifanya hivyo*. Ndiyo kusema maneno hayo yaliyo katika parandesi yanaunda kiambajengo tunachokiita kirai tenzi. Katika muktadha wa sentensi 12a), haiwezekani kubadili *[alichukua vitabu]* na kuacha nje *vilivyobaki mezani* kwa sababu maneno hayo ni sehemu ya kirai nomino kilicho yambwa katika kishazi tegemezi, tungo rejeshi *[vitabu vilivyobaki mezani]*. Kwa hivyo basi, katika muktadha huu sentensi 12d) si sahihi, na kwa hivyo *[alichukua vitabu]* si kiambajengo kinachoweza kubadilishwa na kiwakilishi. Ni muhimu kukumbuka kwamba hapa kinachochunguzwa si kama inawezekana kuunda viambajengo kwa kutumia maneno haya. Kinachochunguzwa ni je, katika miundo tuliyoipata, tunaweza kuzitambua sehemu kuwa ni viambajengo?

## 2.3 Ubadili wa Virai Husishi

Vikundi na virai vinavyoelezea mahali huweza kuwakilishwa na viwakilishi oneshi vya Ngeli za 16, 17 na 18. Kwa mfano:

13 (a) Nilimwona mkurugenzi *[katika ofisi ya mhasibu]*.
(b) Nilimwona mkurugenzi *humo*.

14 (a) Tulikutana *[karibu na duka la dawa]*.
(b) Tulikutana *pale*.

Kikundi cha maneno [*katika ofisi ya mhasibu*] katika sentensi 13a) kimebadilishwa na *humo* katika 13b). Jambo hili linaonekana pia katika mifano inayofuata. Sentensi 14a) ina kikundi [*karibu na duka la dawa*], ambacho kinawakilishwa na *pale* katika sentensi 14b). Waweza kuona kwamba katika fasili iliyo sahihi ya sentensi hizi, haiwezekani kusema **Nilimwona mkurugenzi humo ya mhasibu*. Wala hatuwezi kusema **Tulikutana pale dawa* kwa matarajio kwamba *pale* inawakilisha [*karibu na duka la*]. Hiki si kiambajengo. Hiki hakiwezi kuwa kiambajengo mpaka kikamilike na kuwa [*karibu na duka la dawa*].

## 2.4 Ubadili wa Vishazi

Si virai tu vinavyoweza kutathminiwa na kuthibitishwa kwa kigezo cha ubadili na kuwakilishwa na viwakilishi oneshi. Hata vishazi ni viambajengo vinavyoweza kubadilishwa na viwakilishi oneshi. Katika mifano ifuatayo tunajaribu kutumia kigezo hiki ili kubainishia viambajengo vinavyounda sentensi zenye mchangamano wa viwango mbalimbali.

15 (a) Alisema *[atawachukulia hatua rafiki zake]*.
(b) Alisema *[hivyo]*.

16 (a) [Pele alikuwa mchezaji bora kuliko Maradona].
(b) [Hiyo] ni kweli.

Sentensi 15a) imeundwa na kishazi kikuu chenye kitenzi *alisema*. Kijalizo cha kitenzi hiki ni kishazi tegemezi [*atawachukulia hatua rafiki zake*]. Kishazi tegemezi hiki kinawakilishwa na *hivyo* katika sentensi 15b). Jambo hili linaonekana tena katika jozi iliyopo katika 16). Hapo tunaona kwamba kishazi huru chote kilicho katika 16a) kinawakilishwa na *hiyo* katika 16b). Ndiyo kusema, sentensi 16b) inasema kwamba [*Pele alikuwa mchezaji bora kuliko Maradona*] *ni kweli*. Katika mfano wa kwanza 15), *hivyo* haiwezi kuwakilisha **[hatua rafiki zake]* kwa sababu *hatua* hapa ni sehemu ya nahau ambayo ni *chukua hatua*. Katika kutenganisha kitenzi na kijalizo chake cha kinahau tumeweza kuona kwamba tumekivunja kishazi kwa namna isiyotupa viambajengo.

**3. Usogezaji**

Ugeuzaji ni dhana muhimu sana katika nadharia ya sarufi ya kisasa hasa sarufi zalishi. Nadharia ya ugeuzaji miundo imetumika hasa toka kuchapishwa kwa *Syntactic Structures* cha Chomsky (1957). Miongo mingi imepita na hata muasisi mwenyewe amebadilisha mtazamo na istilahi nyingi za nadharia yake (Chomsky 2001). Hata hivyo usogezaji ni dhana inayobaki kuwa muhimu sana kwa wanasintaksia wengi wa leo. Katika sehemu hii tutatumia kanuni usogezaji kuthibitisha viambajengo. Katika mtazamo huu wa sarufi, sentensi hizi zifuatazo zina uhusiano wa moja kwa moja.

17 (a) Watoto walimvuta mbuzi.
(b) Mbuzi alivutwa na mtoto.

Kwa msemaji yeyote wa Kiswahili, sentensi hizi zina wahusika wale wale, wakati wa tukio unaosemwa ni ule ule, na tendo linalotendwa ni lile lile. Sentensi hizi zina maana ile ile. Lakini katika 17a), msemaji ameweka *watoto* kama kiima na *mbuzi* kama yambwa. Tunajua kwamba *watoto* ni kiima kwa sababu tunaona upatanisho wa kisarufi unaofanywa na kiambishi *wa-* kwenye kitenzi. Hali kadhalika, -*m*- katika kitenzi inaashiria kwamba *mbuzi* ni yambwa. Katika sentensi 17b), *mbuzi* ni kiima. Jambo hili linadhihirika hasa unapoangalia kitenzi ambacho sasa kina kiambishi awali cha *a-*, ambacho kinapatana na *mbuzi*. Sentensi 17a) iko katika kauli ya utendi, na sentensi 17b) iko katika kauli ya utendwi (utendwa). Katika nadharia ya ugeuzaji,

sentensi ya utendwi imetokana na kugeuza muudo wa sentensi ya utendi. Kuna mdahalo mkubwa miongoni mwa wanasarufi juu ya jambo hili. Katika makala hii tunatilia umuhimu hasa uhusiano wa sentensi hizi mbili kimuundo.

Kimuundo, kuna mambo mawili muhimu katika tafsiri ya viambajengo na virai.
Jambo la kwanza ni nadharia ya ugeuzaji inavyoelezea uhusiano wa sentensi mbili zenye maana zinazohusiana. Hebu tuione dhana hii katika mifano halisi ifuatayo.

18 (a) Juma alinunua *[kitabu cha fasihi]*.
(b) [*Kitabu cha fasihi*] Juma alinunua.

Sentensi iliyo katika 18a) ina mpangilio wa Kiima-Kitenzi-Yambwa, mpangilio ambao unafahamika kama wa kawaida katika lugha hii (Ashton, 1947; Krifka, 1995; Mohammed, 2001). Sentensi 18b) ina mpangilio tofauti na hiyo ya kwanza, yaani, Yambwa-Kiima-Kitenzi. Wanasintaksia wanapendelea kuutambua mpangilio wa 18a) kama ndiyo wa msingi zaidi. Mpangilio tofauti ulio katika 18b) ambao haubadilishi maana unatokana na kusogeza yambwa kutoka mahali pake baada ya kitenzi na kuipeleka mwanzoni mwa sentensi kabla ya kiima. Dhana ya usogezaji, basi, inatusaidia kwanza kutambua kuwa, sentensi hizi mbili zina maana moja, na pili uhusiano wa nafasi mbili wa yambwa ndio unaoelezewa kama usogezaji au uhamishaji. Kama tunatumia uhusika, tunabakiwa na wahusika wale wale. *Juma* ni mtendi ambaye anasababisha kuwa na upatanisho wa kisarufi wa kiima *a-* kwenye kitenzi na inatangulia kitenzi. Yambwa *kitabu cha fasihi* imehamia mwanzoni mwa sentensi.

Jambo la pili ni kwamba tafsiri ya kirai hupatikana mahali ambapo kirai kinachotafsiriwa kimeshahama (taz: Carnie 2013, Cook na Newson 2007, Radford 1988). Ugeuzaji au usogezaji tunauona sana katika kauli ya kutendwa, kauli ya kutendeka, tungo rejeshi, na nyingine nyingi.

Usogezaji unawezekana tu kwa makundi ya maneno yanayounda virai au viambajengo. Mifano yetu hapo juu 18) inaonesha kikundi cha maneno matatu, *kitabu cha fasihi*, ambacho ndiyo yambwa, kinasogea. Hebu tujaribu kuhamisha visehemu vingine ambavyo si viambajengo ili tuone matokeo yake. Tunajua yambwa *kitabu cha fasihi* ni kiambajengo. Ndani yake kuna muundo tena.

19 (a) Juma alinunua *[kitabu cha]* fasihi.

(b) *[Kitabu cha] Juma alinunua fasihi[4].

Katika mfano wa pili 19b), tumejaribu kuweka katika fokasi sehemu tu ya yambwa *kitabu cha*, kitu ambacho hakikubaliki. Ndiyo kusema, kirai *kitabu cha fasihi* hakiwezi kugawanywa katika viambajengo *kitabu cha* na *fasihi*. Katika sehemu hii tunaonesha jinsi ambayo viambajengo vinahamishwa na si sehemu yake au kwa kuambatana na kitenzi kingine.

Miongoni mwa mifano ya mwanzo iliyosababisha kuelezea nadharia ya isimu zalishi ni muundo wa kauli ya kutendwa. Katika kauli ya kutendwa, muathirika huhamishiwa mwanzoni mwa sentensi na kuwa kiima. Wakati huo huo, mtendi huteremshwa na kuwa yambwa ya kihusishi kama tunavyoonesha kwa mifano hii:

20 (a) Maji yalisomba *[magogo]*.
(b) *[Magogo]* yalisombwa na maji.

Kuna wahusika wawili katika sentensi hii, kwa maana ya pande mbili zinashohusika katika tukio la *kusomba*[5]. Wa kwanza ni *maji* ambayo ndiyo yanayofanya kitendo kinachowakilishwa na kitenzi *–somba*. Wa pili ni *magogo* ambayo ndiyo yaliyoathiriwa na tukio hilo. Sentensi 20a) ni katika kauli ya kutenda, na 20b) ni kauli ya kutendwa. Kimsingi sentensi hizi mbili zina maana sawa. Tukichukulia 20a) kuwa ndiyo hasa ya msingi, tunaona kwamba sentensi 20b) inatokana na kuhamisha neno *magogo* na kulifanya kiima.

Muundo huu basi unaweza kutumika kubainisha viambajengo ambavyo ni yambwa katika sentensi.

21 (a) Maji yalisomba [*magogo yaliyolala karibu na mto*].
(b) [*Magogo yaliyolala karibu na mto]* yalisombwa na maji.
(c) *[*Magogo*] yalisombwa yaliyolala karibu na mto na maji.
(d) *[*Magogo yaliyolala*] yalisombwa karibu na mto na maji

Jaribio letu katika 21) limebainisha kwamba *magogo yaliyolala karibu na mto* ni kiambajengo katika sentensi hii kama kilivyohamishwa katika 24 (b). *Magogo*

4 Tunajua kwamba kipashio *[kitabu cha fasihi]* kina muundo tena ndani yake. Hatutauangalia muundo huu hapa.

5 Tunatumia *uhusika* kwa maana ile inayotumika na wengine kama Khamis (2008) na hata uhusika inavyotumika katika Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha (TUKI 1990)

*yaliyolala* si kiambajengo kamili katika muktadha wa sentensi yetu ya msingi na inavyodhihirishwa katika kushindwa kugeuza 24 (d).

Ugeuzaji kama wa kauli ya kutendwa huonekana pia katika kauli ya kutendeka. Kauli ya kutendeka hupatikana katika lugha nyingi za Kibantu zikiwemo Chichewa (Mchombo 1993), na Kinyamwezi (Lodhi 2002). Tofauti na kauli ya kutendwa, kauli ya kutendeka kwa hakika haimtaji mhusika aliyeathiriwa. Kwa mfano, katika Kiswahili tunasema:

22 (a) Mafuriko yalibomoa daraja la dharura.
(b) Daraja la dharura lilibomoka.

Katika sentensi 25 (a), kitu kilichobomoa daraja kinatajwa kama kiima *mafuriko*. Nafasi yake kama kiima inadhihirika katika kiambishi awali cha kiima *ya-* kinacho-patana na ngeli hiyo ya mafuriko. *Daraja la dharura* ni yambwa katika sentensi 22a). Katika sentensi 22b), kihusika hiki ndicho kiima na kinakaa mwanzoni mwa sentensi. Upatanisho wa kisarufi wa kiima pia unapatana na kiima *daraja* chenye kiambishi *li-* kwenye kitenzi. Katika mazingira haya tunasema, kihusika hiki kimehamia katika nafasi ya kiima.

Tunapokuwa na virai virefu zaidi, ni rahisi kuchanganya mambo na kusahau kirai kinaanzia wapi na kinaishia wapi. Njia hii ya usogezaji inaweza kusaidia sana katika kubainisha mipaka ya viambajengo. Kwa mfano, angalia sentensi hizi:

23 (a) Tulimpata [*mtu wa kununua mkweche wetu*].
(b) [*Mtu wa kununua mkweche wetu*] alipatikana.
(c) *[*Mtu wa kununua alipatikana*] mkweche wetu.
(d) *[*Mtu wa*] alipatikana kununua mkweche wetu.

Katika sentensi 26 (a), yambwa *mtu wa kununua mkweche wetu* inaonekana baada ya kitenzi. Kwa kutumia muundo wa kauli ya kutendeka, kiambajengo hicho kinaweza kuhamishiwa mwanzoni mwa sentensi, kama inavyooneshwa katika 26 (b). Tunapo-jaribu kusogeza sehemu tu ya kiambajengo hiki bila kujali mipaka yake ndipo tunapopata sentensi zisizokubalika kama 26 (c) and 26 (d). Ndiyo kusema, kwa mujibu wa sentensi yetu ya msingi 26 (a), *mtu wa kununua* haiwezi kuwa kiambajengo mbali na *mkweche wetu*. Hali kadhalika, *mtu wa* katika 26 (d) haiwezi kuwa kiambajengo.

Muundo mmoja rahisi kutumika katika kubainisha viambajengo ni fokasi. Katika muundo huu, virai mbalimbali vyaweza kuhamishiwa mwanzoni mwa sentensi ili

kuvipa mwonekano zaidi. Ndiyo kusema kikundi cha maneno kikiweza kuhamishwa bila kubadilisha maana ni kiambajengo. Kikundi husishi katika sentensi ya kwanza hapo chini chaweza kuhamishwa kama inavyooneshwa katika sentensi ya pili.

24 (a) Walikaa [*chini ya miti*] wakazungumza.
(b) [*Chini ya miti*] walikaa wakazungumza
(c) *[*Chini ya*] walikaa mti wakizungumza.

Kirai kizima kinapohama, kama inavyoonekana katika 24(b), tunapata sentensi sahihi. Uhamishaji huu ukihusisha sehemu tu ya kirai hiki, basi matokeo yake si sentensi inayokubalika, kama tunavyoona katika 27 (c) ambapo yambwa ya kihusishi haikuhama pamoja na sehemu nyingine za kiambajengo hicho.

**4. Majibu Mafupi na Udondoshaji**

Ijapokuwa tunapoandika, kwa mfano, makala kama hii, tunatumia sentensi kamili, katika lugha ya mazungumzo aghalabu tunatumia sana vifupisho vya sentensi. Miongoni mwa vifupisho hivyo ni majibu mafupi, na vifupisho vingine ni vya udondoshaji. Katika sehemu hii tutaonesha jinsi vifupisho hivi vinavyodhihirisha uambajengo.

**4.1 Majibu Mafupi**

Majibu mafupi kwa maswali ya umbomaana ni kipimo kizuri pia cha kubainisha mshikamano wa viambajengo. Tofauti na maswali yanayotaka majibu ya *ndiyo* au *hapana*, maswali ya umbomaana hudai majibu ambayo yanaleta habari. Kwa mfano:

25 (a) Ulinunua nini jana?
(b) [*Daftari la mazoezi ya isimu*].

26 (a) Ulisaidiana na nani?
(b) *[Msichana mwenye miwani myeusi]*.

Jibu linaloonekana katika 28 (b) si sentensi kamili lakini ni jibu toshelevu la swali la 28a. Hakuna kiarifu katika jibu hili. Lakini kikundi hiki cha maneno kinakubalika kabisa katika lugha ya kawaida ya mazungumzo. Kukubalika kwake ni ushahidi tosha kwamba ni kirai chenye mshikamano. Jambo hili pia linadhihirika katika jozi ya tungo 26).

## 4.2 Udondoshaji

Udondoshaji ni kigezo kimojawapo kinachoweza kutumika katika kubainisha viambajengo. Mifano mizuri sana ya mchakato huu hupatikana katika sentensi ambazo zina sehemu zilizo sawa ambapo ya pili ikidondoshwa maana yake huelekezwa na ile ambayo imebaki (Haegeman, 2006; Carnie, 2013; Radford, 1988; Ngonyani, 1996). Jambo hili linadhihirika katika mifano ifuatayo.

27 (a) Amina amenunua *[shamba la katani]* na
Athmani amenunua *[shamba la katani]* pia.

(b) Amina amenunua *[shamba la katani]* na Athmani amenunua pia[6].

Katika mfano 27a), kuna vishazi viwili huru ambavyo vimeunganishwa na kiunganishi *na*. Vishazi vyote viwili vina yambwa *[shamba la katani*]. Wasemaji wa Kiswahili wanaweza kusema *pia* kama ilivyo katika 30 (b) ambapo yambwa hiyo shirika haijarudiwa. Jambo muhimu la kukumbuka hapa ni kwamba udondoshaji huu huhusu viambajengo. Makundi ya maneno ambayo hayaundi viambajengo hayadondoshwi hivyo, kama tunavyoona katika mifano hii.

28 (a) Halima amekata miti ya kujengea daraja na
Omari [amekata] pia.

(b) *Halima amekata miti ya kujengea daraja na
Omari kujengea daraja pia.

Kirai nomino *[miti ya kujengea daraja]* kinaonekana katika kishazi cha kwanza cha 31 (a) lakini hakipo katika kishazi cha pili. Hata hivyo wasemaji wa Kiswahili watatambua kwamba yambwa hiyo hiyo ndiyo inayokamilisha kikundi tenzi cha kishazi cha pili. Katika mfano wa 31 (b), **[amekata miti ya]* kimedondoshwa kutoka kishazi cha pili. Walakini matokeo yake ni sentensi isiyokubalika. Kikundi hiki si kiambajengo katika muktadha huu.

## 5. Uambatishaji

Uambatishaji hutokea pale neno au makundi ya maneno vyenye hadhi sawa yanapounganishwa kwa kutumia viunganishi. Viunganishi vitumikavyo hasa ni *na, lakini,*

---

6 Baadhi wa wazungumzaji wa Kiswahili hutilia shaka usahihi wa sentensi zenye udondoshaji kama hizi. Shaka hilo lazima likumbukwe.

*bali, au*, nk. Uambatishaji huhusu viambajengo vya namna moja. Hebu tuangalie mifano ifuatayo ambamo kwa kutumia mabano tumeonyesha viambajengo vinavyo-ambatishwa.

29 (a) [Neema anaandika insha] na [Kazimoto anapika chakula].
(b) Neema ataanza [*kuandika insha*] na [*kuandaa madarasa*].
(c) Tulitoa hoja *[katika mikutano]* na *[katika makongamano]*.
(d) Athmani ni kijana [*mrefu*] lakini [*mvivu*].
(e) [*Mtoto wa Neema*] na [*mgeni wa Kazimoto*] wameondoka.

Katika 29a), vishazi huru viwili vimeambatishwa kwa kutumia kiunganishi *na.* Viambajengo vilivyounganishwa katika 29b) ni virai tenzi. Sambamba na muundo huo tunaona pia katika 29c) kwamba vikundi husishi viwili vimeambatishwa. Vivumishi viwili vimeambatishwa kwa kutumia kiunganishi *lakini* katika sentensi 29d). Virai nomino ndivyo vinavyofanya yambwa ambatani katika 29e).

Mifano yote inaonesha sifa hiyo muhimu ya viambajengo ambatani, nayo ni kwamba virai huambatishwa na virai, virai tenzi huambatishwa na virai tenzi, virai vumishi huenda na virai vumishi, virai nomino na virai nomino, n.k. Kwa hivyo basi, iwapo unaweza kuambatisha kikundi cha maneno kwa kirai fulani, basi kikundi hicho kina hadhi ya kiambajengo.

(30) (a) *Neema [*anaandika insha*] na [*katika nyumba*].
(b) *[*Wanafunzi wa Kiswahili*] na [*polepole sana*] watagoma.

Katika mfano wa kwanza (30a), kiunganishi a kinaambatisha KN *[insha]* au KT *[anaandika insha]*, na KH *[katika nyumba]*. Sentensi hii haikubaliki. Kadhalika, jambo hili linadhihirika katika (30b) ambapo KN *[wanafunzi wa Kiswahili]* na KE *[polepole sana]* vinaunganishwa na kuleta tungo isiyokubalika.

Jambo la msingi linalooneshwa hapa ni kwamba virai vya kategoria tofauti haviwezi kuambatishwa kwa kutumia viunganishi. Endapo tunaweza kuunganisha makundi ya maneno kwa kutumia viunganishi hivyo basi, tunajua kwamba hapo tuna viambajengo vyenye hadhi na kategoria sawa.

**6. Mifano ya Matumizi Katika Utafiti**

Njia hizi jarabati hutumika sana katika kuchanganua muundo wa sentensi. Umuhimu huo tutauonyesha katika kutathmini mapendekezo ya miundo mbalimbali. Kwanza tutatathmini muundo wa sentensi tuliouona katika kitabu cha Besha (1994). Pili

tutajaribu kuchanganua muundo wa tungo zenye yambwa mbili, kama tungo za kutendea. Tatu tutachanganua utata utokanao na muundo.

**6.1 Muundo wa Sentensi za Kiswahili**

Tuanze kwa kurudia swali tulilolizua mwanzoni mwa makala. Je, twawezaje kuthibithisha kwamba mchanganuo mmoja wa sentensi ni sahihi na si mwingine. Kwa mfano, baina ya 34 (a) na 34 (b), tunatathmini vipi mchanganuo?

31 (a) [mtoto mdogo] [ameleta [machungwa matamu]]
(b) [mtoto mdogo] [ameleta] [machungwa matamu]

Miundo hii imewasilishwa katika vielelezo matawi **Error! Reference source not found.**) na 1) hapo juu. Tunachukulia miundo hiyo miwili kama nadharia tete mbili tofauti. Tutatumia mbinu zetu kuthibitisha au kukanusha nadharia tete hizo.

Hebu tuanze na muundo 31b) ambao unaonesha kwamba sentensi hii imeundwa kwa viambajengo vitatu, navyo ni (i) kirai nomino – *[mtoto mdogo]*, (ii) kitenzi – *[ameleta]*, na (iii) kirai nomino - *[machungwa matamu]*. Hii ina maana kwamba kitenzi kilichopo hakiundi kiambajengo na kirai nomino cha pili. Kitenzi kiko peke yake na kirai nomino kiko peke yake. Ndiyo kusema nadharia tete hii inatabiri kwamba huwezi kutumia vigezo tulivyoviona hapo juu na kukuta kitenzi hicho kinaunda kirai au kiambajengo na kikundi nomino kinachofuatia, isipokuwa kama unaichukulia sentensi nzima. Je, jambo hili ni kweli? Tunatumia majibu mafupi na ubadili kuthibitisha kwamba hivyo sivyo.

32 (a) mtoto mdogo amefanya nini?
(b) [*ameleta machungwa matamu*].


33 (a) Nani ameleta machungwa matamu?
(b) Mtoto mdogo [*amefanya hivyo*].

Jibu fupi katika 35 (b) ni kitenzi pamoja na kirai nomino. Ushahidi huu unapata nguvu zaidi kutoka 36 (b) ambapo tunaona kwamba *[amefanya hivyo]* inawakilisha *[ameleta machungwa matamu]* pia. Matokeo haya yanabatilisha kabisa nadharia tete iliyo katika muundo wa 31 (b). Wakati huohuo yanathibitisha muundo ulio katika nadharia tete 34 (a), na ni ule ambao tulitaja mwanzoni kuwa baadhi ya wanasintaksia ya Kiswahili huukubali (Besha, 1994; Massamba, Kihore, & Hokororo, 1999; Matinde, 2012).

**6.2 Yambwa katika Kauli ya Kutendea**


Mfano mwingine mzuri sana wa matumizi ya vigezo na majaribio haya ni katika utafiti wa muundo wa vitenzi vyenye yambwa mbili kama katika sentensi zenye kauli ya kutendea au kutendesha. Hapo nyuma, baadhi ya watafiti wa sentensi za kutendea zenye yambwa mbili walipendekeza kwamba muundo wake ungekuwa kama hivi, kama ilivyopedekezwa na Baker (1988)[7]:

34 (a) Mgeni aliwaletea watoto zawadi.





Uchambuzi huu unaonesha kwamba yambwa zote mbili zina uhusiano sawa na kitenzi maana zote ziko katika ngazi moja. Je, tunaweza kubainisha kwamba huo ndiyo muundo wake? Kwa kutumia udondoshaji, Ngonyani (1996) anaunda nadhariatete na kusema kwamba iwapo muundo wa KT ni wa matawi matatu hivyo, basi udondoshaji utaondoa KT chote mara moja. Katika matumizi ya kipimo hiki, Ngonyani anadai kwamba udondoshaji unaoondoa yambwa katika Kiswahili ni sawa na udondoshaji wa vikundi tenzi kama unavyopatikana katika Kiingereza na Kijapani. Anathibitisha kwa mifano kwamba katika lugha zote hizo kuna sifa zinazopambanua mchakato huu. Hoja hiyo si muhimu katika maelezo yetu ya hapa. Msomaji anaweza kujiridhisha kwa kusoma tasnifu hiyo au makala ya Ngonyani (2000). Tunaridhika na kuangalia udondoshaji kuwa ni wa kiambajengo cha yambwa. Kwetu yatosha kuangalia yambwa zinavyodondoshwa. Muundo wa matawi matatu ya kikundi tenzi cha kutendea kinatabiri kikonyo kimoja tu cha udondoshaji. Ndiyo kusema, udondoshaji unawezekana kwa yambwa zote kwa mpigo tu, na si kudondosha moja na kubakiza nyingine.

35




---

[7] Hili ni pendekezo la zamani. Wakati huo miundo ya matawi matatu ilikuwa bado inakubalika miongoni mwa wataalamu wengi wa mkabala wake Baker. Tasnifu ya Baker (1988) ilikuwa na hoja zilizoweka msingi thabiti wa maingiliano muhimu ya mofolojia na sintaksia.





Nadhariatete hii ilibainishwa kwamba si sahihi. Kwa kutumia sentensi zifuatazo tunaweza kuona mantiki yake kama inavyochorwa na Ngonyani kwa kutumia sentensi za Kindendeule (1996:96-97). Tunazitafsiri sentensi hizo kwa Kiswahili na kupata matokeo yanayofanana.


36 (a) Babu hununulia shule vitabu na bibi hununulia shule vitabu pia.
(b) Babu hununulia shule vitabu na bibi hununulia shule ~~vitabu~~ pia.
(c) *Babu hununulia shule vitabu na bibi hununulia ~~shule~~ vitabu pia
(d) Babu hununulia shule vitabu na bibi hununulia ~~shule vitabu~~ pia.

Jaribio la udondoshaji linalenga kishazi cha pili baada ya kiunganishi. Kishazi hiki kina yambwa mbili kama kilivyo kishazi cha kwanza. Kudondosha kishazi kiathirika, kama inavyooneshwa katika 36 (b), ni sawa na tunapata sentensi sahihi. Jambo hili peke yake linakanusha nadharia tete inayowakilishwa na kielelezo 35b) hapo juu chenye matawi matatu. Isitoshe, katika 39 (c), tunaona kwamba hatuwezi kudondosha yambwa inayofaidika na kitendo cha kitenzi. Mwisho tunaona kwamba yambwa zote mbili zinaweza kudondoshwa pamoja.

Matokeo haya ya jaribio la udondoshaji yana tafsiri moja tu nayo ni kwamba, yambwa mbili hizo haziko katika kikonyo kimoja. Moja iko juu zaidi ya nyingine. Ngonyani (1996: 98) anahitimisha kwamba muundo wa hali ya kutendea ni kama ulivyo katika kielelezo kifuatacho kwa muundo wa X'.

(37)






Uchambuzi huu unaendana vema sana na mapendekezo yaliyotolewa na wanaisimu wengine waliochunguza sentensi zenye yambwa mbili katika lugha nyingine kama vile Kiingereza[8]. Larson (1988) na Marantz (1993) walichunguza uhusiano wa kisintaksia baina ya yambwa mbili hizo wakaonesha kwamba yambwa ya mwathirika huundiwa chini zaidi ya yambwa ya mpokeaji au anayefaidika.

### 6.3 Tungo Tata

Tungo tata ni tungo ambazo zinaweza kupata tafsiri zaidi ya moja. Utata huo unaweza kutokana na maneno yanayotumika katika sentensi, maneno yenye uhusiano wa homonimia. Utata mwingine hutokana na muundo wa sentensi. Aina ya kwanza ya utata inaonekana katika mifano ifuatayo.

38 (a) Alipata taa sokoni.
(b) Tuliiona mito mingi.

Sentensi 38 (a) ni tata kwa sababu tunaweza kutafsiri kwamba *taa* ni mnyama wa baharini au *taa* ni chombo cha kuleta mwanga. Hali kadhalika sentensi 38b) inaweza kueleweka kwamba msemaji anamaanisha waliona *mito* ambayo ni mitiririko mikubwa ya maji, au waliona *mito* ambayo ni kitu cha kuegemezea kichwa kitandani. Kwa maana zote mbili, sentensi itachambuliwa na muundo ule ule. Huu ni utata wa kileksia.

Utata wa kimuundo ni tofauti na utata wa kileksia tuliouona hivi punde. Utata huu unaonekana katika sentensi zifuatazo.

39 (a) Tuliamua kuanza mapigano Jumatano.
(b) Asha aliona vichwa na darubini.

Sentensi 42 (a) inaweza kueleweka kwamba (i) *Siku ya Jumatano ndipo tulifanya uamuzi wa kuanza mapigano;* (ii) inaweza kutafsiriwa kwamba *Tuliamua mapigano*

---


8 Tumeweka kielelezo matawi kama kilivyo katika tasnifu yake. Kielelezo chake kinafuata mchanganuo wa sentensi uliopendekezwa na Pollock (1989). Mjadala wa usahihi wa vikonyo mbalimbali si jambo tunaloweza kulifanya hapa.

*yaanze Jumatano.* Utata huu wa kimuundo unatokana na uwezekano wa kielezi *Jumatano* kuvumisha vitenzi viwili, navyo ni *aliamua* na *kuanza*. Tafsiri hizi zinaweza kuoneshwa vizuri kwa kutumia kigezo cha ubadili, kama tunavyoonesha hapa.

40 (a) Sisi tuliamua kuanza mapigano Jumatano.
(b) Sisi tuliamua **hivyo Jumatano**
(c) Sisi tuliamua **hivyo**.

Tafsiri ya kwanza inashabihiana na tunachokiona katika 40b). Kiwakilishi *hivyo* kinasimama badala ya *kuanza mapigano*, kijalizo cha *tuliamua*. Chagizo *Jumatano* hakimo ndani ya kirai tenzi hicho. Hicho ni chagizo cha kirai chenye kiini chake kama *tuliamua*. Tafsiri ya pili inaweka chagizo hicho ndani ya kirai tenzi kilicho ndani. Kiwakilishi hivyo kinasimama badala ya maneno hayo *kuanza mapigano Jumatano*. Utata huo unaoneshwa kwa vielelezo matawi viwili tofauti.

(41) (a)





(b) [$_S$ [$_{KN}$] [$_{KT}$ [$_{KT}$ tuliamua [kuanza mapigano]] [$_{KE}$Jumatano]]]

hivyo

*Jumatano* ni chagizo cha KT chenye kichwa chake *tuliamua*. Kwa hivyo uamuzi ulifanyika Jumatano.

42 (a)




(b) [$_{S}$ [$_{KN}$] [$_{KT}$ tuliamua [$_{KT}$ [$_{KT}$kuanza mapigano] [$_{KE}$Jumatano]]]]

hivyo

*Jumatano* ni chagizo cha kirai chenye kiini chake *kuanza*. Kwa hivyo mapigano yataanza Jumatano.

Kwa hivyo basi, njia za kubaini viambajengo ni mbinu bora kabisa ya kuelezea utata wa kimuundo. Hapa tumetoa mifano michache tu ili kuonesha masuala mbalimbali yanavyoweza kuchunguzwa na miundo inavyoweza kupambanuliwa kwa kutumia vigezo tulivyoelezea hapa. Tunafahamu, kwa mfano, Bresnan & Mchombo (1995) wanatumia vigezo na majaribio haya kuonyesha ambavyo muundo wa maneno hautokani na kanuni na sheria za kisintaksia.

## 7. Hitimisho

Katika makala hii tuliuliza swali la msingi kabisa katika sintaksia, nalo ni je tunawezaje kuthibitisha mchanganuo wa sentensi au vikundi mbalimbali vya maneno. Tulitoa mfano wa jinsi gani tunaweza kubainisha muundo wa kishazi ni? kuwa kina vikonyo sisisi viwili tu? Tumetumia vigezo ambavyo vinatumika na wanaisimu wa mikabala mbalimbali katika kutafiti lugha mbalimbali. Vigezo hivyo ni: (a) kama kikundi cha maneno kinaweza kusimama peke yake kama jibu fupi, hicho ni kiambajengo; kadhalika ni viambajengo tu ndivyo vinavyoweza kudondoshwa; (b) kama kikundi kinaweza kubadilishwa kwa kutumia viwakilishi na vioneshi basi hivyo ni viambajengo pia; (c) kama kikundi cha maneno kinaweza kuhamishwa, kwa mfano katika kauli ya kutendwa, basi ni kiambajengo; na (d) hali kadhalika ni viambajengo vinavyofanana tu ndivyo vinavyoweza kuambatishwa.

Baada ya kutoa maelezo juu ya kila kigezo na kutoa mifano kadha, tukavitumia vigezo katika kuthibitisha na kufafanua mambo matatu muhimu kabisa. Kwanza tumethibitisha kwamba muundo wa sentensi kwa hakika unahusu viambajengo viwili, kiima na prediketa. Kitenzi na kijalizo chake hufanya kiambajengo. Pili tumeangalia matumizi ya vigezo hivyo katika kuchanganua muundo wa vikundi tenzi vya vitenzi vya kauli ya kutendea ambapo yambwa mbili hutokea. Matokeo ya uchunguzi kwa kutumia mbinu hizi umethibitisha yale ambayo baadhi ya wachunguzi waliyabaini, kwamba muundo wa sentensi zenye yambwa mbili ni tangamani zaidi na si wa vikonyo vyenye matawi matatu. Tatu tumeonesha kwamba vigezo hivi vinatoa tafsiri mbili zinazoendana na utata wa kimuundo.

Matumaini yetu ni matumizi zaidi ya njia jarabati katika kuchanganua miundo mbalimbali ya Kiswahili na lugha nyingine. Matumizi ya mbinu hizi ni muhimu katika kujenga ujarabati na usayansi wa isimu. Kuendeleza stadi hii ya uchanganuzi kutasaidia kuifanya isimu kuwa taaluma inayotegemea uchunguzi wa kisayansi zaidi.

## Marejeleo

Aarts, B. (2001). *English Syntax and Argumentation* (2nd ed.). New York: Palgrave Publishers.

Ashton, E. O. (1947). *Swahili Grammar (Including Intonation).* London: Longmans, Green and Co.

Baker, M. (1988). *Incorporation: A Theory of Grammatical Function Changing.* Chicago: Chicago University Press.

Barss, A., & Lasnik, H. (1986). A Note on Anaphora and Double Objects. *Linguistic Inquiry, 17* (2), 347-354.

Besha, R. M. (1994). *Utangulizi wa Lugha na Isimu.* Dar es Salaam: Dar es Salaam University Press.

Bresnan, J. & Mchombo, S. (1995). The lexical integrity principle: evidence from Bantu. *Natural Language and Linguistic Theory, 13*, 181-254.

Bresnan, J. & Mchombo, S. (1987). "Topic, Pronoun and Agreement in Chichewa," *Language, 63*, 741-782.

Carnie, A. (2013). *Syntax: A Generative Introduction* (3rd ed.). Oxford: Wiley Blackwell.

Chomsky, N. (1957). *Syntactic Structures.* The Hague: Mouton.

Cook, V. J. & Newson, M. (2007). *Chomsky's Universal Grammar.* Malden, MA: Blackwell Publishers.

Haegeman, L. (2006). *Thinking Syntactically: A Guide to Argumentation and Analysis.* Oxford: Blackwell Publishing.

Keach, C. N. (1995). "Subject and Object Markers as Agreement and Pronoun Incorporation in Swahili," katika A. Akinbiyi (Mhariri.), *Theoretical Approaches to African Linguistics* (uk. 109-116). Trenton, NJ: Africa World Press.

Khamis, A. M. (2008). *Maendeleo ya Uhusika.* Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Krifka, M. (1995). Swahili. in J. Jacobs, A. von Stechow, W. Sternefeld, & T. Vennemann (Eds.), *Syntax: An International Handbook of Contemporary Research* (Vol. 2, pp. 1397-1418). Berlin: Walter de Gruyter.

Larson, R. (1988). "On double object constructions,"*Linguistic Inquiry, 19*, 335-391.

Lodhi, A.Y. (2002). "Verbal Extensions in Bantu: The Case of Swahili and Nyamwezi,"*Africa and Asia, 2*, 5-26.

Marantz, A. (1993). "Implications of the Asymmetries in Double Object Constructions,"katika S. A. Mchombo (Mh.), *Theoretical Aspects of Bantu Grammar* (uk. 113-150). Stanford: Center for the Study of Language and Information.

Massamba, D.P.B. Kihore, Y. M., & Hokororo, J. I. (1999). *Sarufi Miundo ya Kiswahili Sanifu (SAMIKISA) Sekondari na Vyuo.* Dar es Salaam: Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili.

Matinde, R. S. (2012). *Dafina ya Lugha Isimu na Nadharia.* Mwanza: Serengeti Educational Publishers.

Mchombo, S. (1993). "A Formal Analysis of the Stative Construction in Bantu,"*Journal of African languages and linguistics, 14*, 5-28.

Mohammed, M. A. (2001). *Modern Swahili Grammar*. Nairobi: East African Educational Publishers.

Ngonyani, D. (2000). "The Constituent Structure of Kindendeule Applicatives,"Katika V. Carstens, & F. Parkinson (Wah.), *Advances in African Linguistics* (uk. 61-76). Trenton, N.J.: Africa World Press.

Ngonyani, D. (1996). *The Morphosyntax of Applicatives*. Los Angeles: UCLA Tasnifu ya Shahada ya Uzamivu.

Pollock, J.Y. (1989). "Verb Movement, Universal Grammar, and the Structure of IP,"*Linguistic Inquiry*, *20* (3), 365-424.

Radford, A. (1988). *Transformational Grammar: A First Course*. Cambridge: Cambridge University Press.

Sportiche, D. Koopman, H., & Stabler, E. (2014). *An Introduction to Syntactic Analysis and Theory*. Wiley Blackwell.

TUKI. (1990). *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*. Dar es Salaam: TUKI, Chuo Kikuu cha